

# SIKU NYERERE YA 2023



## Mkataba wa bil 9/- wasainiwa kukabili tabianchi

**Na Lucy Lyatuu**

**S**ERIKALI imesaini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) kwa ajili ya tafiti za kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa ufadhilli unaogharim Sh bilioni tisa.

Makubaliano hayo yaliifikiwa Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu

wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Dk Amos Nungu na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Watu kutoka Balozi za Norway na Sweden, Lisa Sivertsen na kushuhudiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk Sellemanni Jafo akiwa na Balozi wa Norway nchini, Tonne Tines na Balozi wa Sweden, Charlotta.

Jafo alisema makubaliano

hayo yamefikiwa baada ya mkataba uliosainiwa Septemba mwaka huu wa ushirikiano na Norway wa programu ya miaka mitano ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi inayotekelawa na Costech.

Alisema fedha hizo zilitzotolewa na Norway zitatumwi na watafiti nchini kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuangalia namna ya kupunguza athari.

"Athari za mabadi-

liko ya tabianchi ni wazi zinaonekana ikiwamo barafu kuyeyuka, uharibifu wa miundombinu na hata ukame," alisema na kuongeza kuwa ajenda ya tafiti nchini itakuwa kubwa na Sweden pia imekubali kutoa ushirikiano.

Aliwaomba watafiti kujikita kufanya tafiti zenye kuleta tija kwa matatizo yanayoikumba jamii na kwamba kama ni eneo la kilimo hali iweje na pia

miundombinu ujenzi wake uwe wa namna gani.

Kwa upande wake, Nungu alisema fedha zilitzotolewa na Norway zimepitia chini ya mfumo wa Sayansi na Teknolojia ili kufadhili tafiti katika eneo hilo.

Balozi wa Norway, Tinnes alisema ufadhili huo ni sehemu ya makubaliano yaliyofikiwa kwa ajili ya kukubaliana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mradi huo unahusisha tafiti zinazoweza kutoa elimu kuhusu tabianchi ambazo zitawasaidia Watanzania kufahamu kwa kina kuhusu mabadiliko ya tabianchi, athari na namna ya kukabiliana nayo.

Kwa upande wake Balozi wa Sweden, Macias alisema mradi utaongeza uwezo wa Watanzania katika tafiti na kuimarisha taasisi kuhusu tabianchi na kwamba wako tayari kushiriki.

## Samia kuweka jiwe la msingi Barabara ya Itigi - Mbeya

**Na Abby Nkungu, Singida**

**M**APOKEZI makubwa yanamsubiri Rais Samia Suluhu Hassan atakapowasili kesho asubuhi mkoani Singida kwa ziara ya kikazi ya siku tatu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alisema mjini hapa kuwa Rais Samia anatarajiwa kufika Singida akitokea mkoani Manyara na atapokelewa katika Kijiji cha Sagara karibu na mpaka wa mikoa hiyo miwili kwenye Barabara Kuu ya Singida - Arusha kisha kwenda moja kwa moja Manispaa ya Singida na atafungua shule mpya ya msingi ya Imbele.

Ratiba inaonesha siku hiyo pia atasafiri hadi Itigi kuweka jiwe la msingi la Barabara ya Itigi - Mbeya inayojengwa kwa kiwango cha lami kisha kuhutubia wananchi.

Serukamba alisema Rais atasafiri hadi Ikungi na kuzindua vituo vya polisi vya kisasa vya wilaya za Mkalama na Ikungi.

Baadaye Rais atahutubia mukutano wa hadhara katika Kijiji cha Puma akiwa njiani kurejea mjini Singida kwa ajili ya mapumziko mafupi kabla ya kula chakula cha jioni na wazee wa mkoa huu.

Serukamba alisema Oktoba 16, Rais atakwenda kukagua na kuzindua daraja msingi katika Wilaya ya Mkalama.

Kwa mujibu wa ra-

tiba hiyo, Oktoba 17 Rais atasafiri hadi Shelui, Iramba ambako atapokea taarifa ya ujenzi wa umeme kwenye vijiji mbalimbali wilayani humo vinavyojengwa na Wakala ya Nishati Vijiji (REA).

Serukamba alisema Rais Samia atakamilisha ziara yake siku hiyo kwa kuzindua mradi mkubwa wa maji, Tinde - Shelui unaotoka Ziwa Victoria.


"Kutokana na mkoaa kupokea kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakijawahi kuleta kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo, namna pekee ya kuonesha shukrani zetu ni wananchi kujitokeza kwa wingi kumlaki wakati wote atakapokuwa mkoani kwetu," alisitisiza Serukamba.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA  
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



**MIAKA 24  
KUMBUKIZI  
YA KIFO CHA HAYATI MWALIMU J.K. NYERERE**



**Bodi ya wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, familia ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Watanzania wote katika Kumbukizi ya Miaka 24 ya Kifo cha Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.**

**“  
Uadilifu na Ubunifu  
kwa Utoaji Huduma  
Bora kwa Umma ”**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao,  
S. L. P. 2833, Dodoma,  
Simu: +255222129868,  
Nukushi: +255222129878,  
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz,  
Tovuti: www.ega.go.tz

